

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 56 **JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC)** OKTOBA 2025

TUME YA UTUMISHI WA WALIMU YAADHIMISHA SIKU YA MWALIMU DUNIANI KWA KISHINDO



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke akizungumza na vyombo vya habari tarehe 1 Oktoba, 2025 kuhusu shughuli mbalimbali kuelekea kilele cha Siku ya Mwalimu Duniani.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania



[tumeyautumishiwawalimutanzania](https://www.instagram.com/tumeyautumishiwawalimutanzania)

TUSHIRIKIANE NA WALIMU KULEA TAIFA LENYE MAADILI NA UELEWA

Kila mwaka tarehe 5 Oktoba, dunia huadhimisha Siku ya Mwalimu Duniani kama ishara ya kuthamini mchango wa walimu katika kuelimisha, kulea na kujenga jamii yenye maarifa. Maadhimisho haya si tu fursa ya kupongeza kazi ya ualimu, bali ni ukumbusho wa wajibu tulio nao sote kama jamii – serikali, wazazi na wananchi – katika kuhakikisha walimu wanafanya kazi katika mazingira yenye heshima, ushirikiano na weledi.

Walimu wana jukumu kubwa la kuandaa kizazi kijacho, lakini mafanikio ya kazi yao hayawezi kupatikana ikiwa wazazi na walezi wataacha jukumu la malezi mikononi mwao pekee. Elimu bora inajengwa kwa ushirikiano kati ya shule na jamii. Ni wajibu wa kila

mzazi kufuatilia maendeleo ya mwanawe, kuheshimu walimu, na kushirikiana nao katika kuunda tabia, nidhamu na maadili mema.

Vivyo hivyo, walimu na watumishi wa umma kwa ujumla wanapaswa kutekeleza wajibu wao kwa weledi, uadilifu na kujituma. Kila mtumishi anapofanya kazi kwa moyo wa kujitolea, heshima na ufanisi, anachangia ustawi wa taifa.

Kwa hiyo, tuwaheshimu na kuwaunga mkono walimu wetu, tuwathamini kama walinzi wa maadili na maarifa ya taifa. Kwa pamoja, tukiweka uzito katika malezi na elimu, tutajenga taifa lenye maadili, maarifa na mustakabali bora kwa vizazi vijavyo.

KATUNI



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti

Paulina M. Nkwama

Wajumbe

Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya
Edwin Mgendera

Mhariri Mkuu

Artemony T. Vincent

Mhariri

Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa

Lucas G. Ogunde

TUME YA UTUMISHI WA WALIMU YAADHIMISHA SIKU YA MWALIMU DUNIANI KWA KISHINDO

Na Mwandishi Wetu, Dodoma

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeadhimisha Siku ya Mwalimu Duniani kwa kishindo jijini Dodoma kwa kuandaa maonesho ya huduma, vipindi vya ueleimishaji kwenye vyombo vya habari na bonanza la michezo lililowashirikisha walimu, viongozi wa serikali na wadau wa mbalimbali wa elimu.

Maadhimisho hayo yayohitimishwa Oktoba 5, 2025 yaligawanyika katika sehemu mbili tatu — maonesho ya huduma mbalimbali katika Viwanja vya Nyerere Square kuanzia Oktoba 1 hadi 5, 2025, ziara za kutoa elimu kwenye vyombo vya habari na bonanza la michezo lililofanyika katika Viwanja vya Kilimani likihitimisha rasmi maadhimisho hayo kwa shamrashamra, burudani na michezo ya kirafiki.

Mgeni rasmi katika bonanza hilo alikuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dkt. Khatibu Kazungu, akifuatana na viongozi mbalimbali akiwemo Mwenyekiti



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke akizungumza na vyombo vya habari tarehe 1 Oktoba, 2025 kuhusu shughuli mbalimbali kuelekea kilele cha Siku ya Mwalimu Duniani.

wa TSC, Prof. Masoud Hadi Muruke, Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama, Kamishna wa Tume, Bi. Mariam Mnilwa, na Rais wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Dkt.

Suleiman Ikomba.

Walimu na wadau mbalimbali wa elimu kutoka Mkoa wa Dodoma walihudhuria, wakionesha mshikamano na hamasa kubwa ya kusherehekea siku yao.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama akitoa ufafanuzi kwa vyombo vya habari tarehe 1 Oktoba, 2025 jijini Dodoma.

Siku ya Mwalimu Duniani

Siku ya Mwalimu Duniani huadhimishwa kila mwaka tarehe 5 Oktoba, ikiwa ni kumbukumbu ya kutiwa saina kwa Mapendekezo ya mwaka 1966 kuhusu Hali ya Walimu (ILO/UNESCO Recommendation concerning the Status of Teachers). Maadhimisho haya yalianzishwa rasmi mwaka 1994 na UNESCO kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO) kwa lengo la kuenzi mchango wa walimu katika maendeleo ya elimu na jamii.

Malengo makuu ya maadhimisho haya ni pamoja na kutambua mchango wa walimu katika malezi na elimu, kuibua mijadala kuhusu changamoto zao, kuhamasisha vijana kujiunga na ualimu, na kuwapa walimu jukwaa la kujadili mustakabali wa taaluma yao.

TUME YA UTUMISHI WA WALIMU YAADHIMISHA SIKU YA MWALIMU DUNIANI KWA KISHINDO

Kwa mwaka huu, maadhimisho nchini Tanzania yamebebwwa na kaulimbiu isemayo: "Wezesha walimu kuchagua viongozi bora kwa elimu na mafunzo stahiki." Kaulimbiu hii inalenga kuhamasisha walimu kushiriki kikamilifu katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, ili kuchagua viongozi watakaoweka kipaumbele katika sekta ya elimu.

Tume ya Utumishi wa Walimu – Mhimili wa Ustawi wa Walimu

Tume ya Utumishi wa Walimu ni chombo cha kisheria kilichoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu, Sura ya 448, chenye jukumu la kusimamia ajira, maadili na maendeleo ya walimu wa shule za msingi na sekondari Tanzania Bara.

Tume ina ofisi 139 katika ngazi ya wilaya, huku makao makuu yake yakiwa Mtaa wa Mtendeni, jijini Dodoma. Kazi zake kuu ni pamoja na kuthibitisha ajira za walimu, kuwabadilishia vyeo, kupandisha cheo, kusimamia nidhamu na kutoa vibali vya kustaafu au kujiendeleza kielimu.

Katika utekelezaji wa majukumu hayo, Tume hutumia miongozo na waraka wa Serikali, ikiwemo Waraka



Viongozi mbalimbali waliohuduhuria Mkutano na vyombo vya habari uliofanyika katika Ofisi za TSC jijini Dodoma wakisikiliza maswali kutoka kwa waandishi wa habari (harwapo pichani).

wa Maendeleo ya Utumishi Na. 1 wa mwaka 2014, unaoelekeza kanuni na vigezo vya ajira na kupandishwa vyeo. Aidha, Tume hutoa mafunzo elekezi kwa walimu wapya na waliopo kazini kuhusu maadili na maendeleo yao kiutumishi.

Maonesho na Bonanza

Tume iliandaa maonesho ya huduma mbalimbali katika Viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma kuanzia Oktoba 1 hadi 5, 2025. Maonesho hayo yalikusisha wadau muhimu wa elimu na taasisi za kijamii, zikiwemo Ofisi ya Rais – Menejimenti

ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Wizara ya Elimu, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (PSSSF), Benki ya CRDB, na Wakala wa Huduma ya Damu Salama.

Huduma zilizotolewa ni pamoja na ushauri wa kiutumishi, huduma za kifedha, elimu ya hifadhi ya jamii na uchangiaji damu kwa hiari, ikiwa ni sehemu ya kuchochea utu na ubinadamu katika jamii.

Shamrashamra za maadhimisho zilikamilishwa kwa Bonanza la michezo katika Viwanja vya Kilimani, lililojumuisha michezo mbalimbali kama mpira wa miguu, mpira wa pete, riadha, kuvuta Kamba, mbio za magunia, kukimbiza kuku, nk Bonanza hilo lililenga kuimarisha afya, urafiki na umoja miongoni mwa walimu na wadau wa elimu.

Maadhimisho ya mwaka huu yamekuwa ni kielelezo cha namna walimu wanavyothaminiwa kama mhimili wa elimu na maendeleo ya taifa. Kupitia maonesho na bonanza la kitaifa, Tume ya Utumishi wa Walimu imeonesha dhamira ya dhati ya kuwatambua, kuwaenzi na kuwawezesha walimu kuboresha taaluma yao na maisha yao kwa ujumla.

Kwa taarifa zaidi kuhusu huduma za Tume, tembelea tovuti rasmi: www.tsc.go.tz



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (kulia) akiwa na Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama wakiwa katika maonesho ya Siku ya Mwalimu Duniani katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma.

TUME YA UTUMISHI WA WALIMU YAADHIMISHA SIKU YA MWALIMU DUNIANI KWA KISHINDO



Huduma zikiendelea kutolewa katika maonesho ya Siku ya Mwalimu Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma.



Wadau mbalimbali wa elimu wakiwa katika mazoezi ya kukimbia wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani tarehe 5 Oktoba, 2025 jijini Dodoma.

TUME YA UTUMISHI WA WALIMU YAADHIMISHA SIKU YA MWALIMU DUNIANI KWA KISHINDO



Burudani mbalimbali zikiendelea katika Kilele cha Siku ya Walimu Duniani tarehe 5 Oktoba, 2025 katika vizwanja vya Kilimani jijini Dodoma.



Washiriki wa bonanza wakiwa katika viwanja vya Kilimani jijini Dodoma katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani tarehe 5 Oktoba, 2025.

MENEJIMENTI YA TUME YASHIRIKI KUTOA MAONI KUBORESHA RASIMU YA MPANGO MKAKATI

Na Mwandishi wetu, Dodoma.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) tarehe 19 Septemba 2025 imefanya kikao cha menejimenti yake kwa lengo la kutoa maoni juu ya rasimu ya Mpango Mkakati wa miaka mitano 2026/27 – 2030/31 unaotarajiwa kuanza kutumika kuanzia Julai 2026.

Kikao hicho kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Tume kilitoa fursa kwa Wajumbe wa Menejimenti kutoa maoni na mapendekezo yenye lengo la kuboresha rasimu ya mpango huo, hatua iliyoonesha ushirikiano na uwazi katika kupanga mpango wa taasisi.

Rasimu ya mpango huo inaandaliwa kwa kushirikiana na Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP), taasisi yenye uzoefu mkubwa katika masuala ya mipango na maendeleo. Ushirikiano huo unalenga kuhakikisha mpango unakuwa wa kitaalamu, unaotekelezeka na wenye mwelekeo wa muda mrefu.

Akizungumza katika kikao hicho, Mwl. Nkwama alisisitiza kuwa mpango mkakati ni dira ya taasisi, unaotoa mwongozo wa namna rasilimali zinavyotumika, namna ya kupima mafanikio na kuongeza uwajibikaji. "Kupitia mpango huu, tunatarajia kuboresha zaidi huduma zetu kwa walimu nchini," alisema.

Wataalamu wa IRDP walifafanua kuwa taasisi isiyokuwa na mpango mkakati mara nyingi hukosa mwelekeo na hupata changamoto katika utekelezaji. Kupitia hatua hii ya kukusanya maoni, TSC imeweka msingi wa kuhakikisha mpango huo unakuwa nyenzo ya mabadiliko chanya na mafanikio ya muda mrefu.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiongoza kikao cha Menejimenti ya TSC cha kutoa maoni ya kuboresha rasimu ya Mpango Mkakati wa Tume tarehe 19 Septemba, 2025 jijini Dodoma.

MENEJIMENTI YA TUME YASHIRIKI KUTOA MAONI KUBORESHA RASIMU YA MPANGO MKAKATI



Mtaalamu wa kuandaa mpango mkakati kutoka Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP), Dkt. Titus Mwageni a k i z u n g u m z a wakati wa kikao cha menejimenti ya TSC cha kutoa maoni ya kuboresha Mpango Mkakati wa Tume tarehe 19 Septemba, 2025 jijini Dodoma.



Kikao cha Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu cha kuboresha rasimu ya Mpango Mkakati wa Tume kilichofanyika tarehe 19 Septemba, 2025 kikiwa kinaendelea.

DKT. KAZUNGU AWAPONGEZA WALIMU KWA KUJITOIA KUKUZA ELIMU – ATOA WITO WA KUCHAGUA VIONGOZI BORA WANAOSIMAMIA SEKTA YA ELIMU

Na Mwandishi Wetu, Dodoma.

Maadhimisho ya kilele cha Siku ya Mwalimu Duniani yamefanyika kwa shamrashamra kubwa katika Viwanja vya Kilimani jijini Dodoma tarehe 5 Oktoba, 2025.

Maadhimisho hayo yalihudhuriwa na walimu kutoka Wilaya za Mkoa wa Dodoma, Viongozi wa Serikali, Chama cha Walimu (CWT) ngazi ya Mkoa na Taifa pamoja na wadau mbalimbali wa elimu.

Mgeni rasmi, Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dkt. Khatibu Kazungu, akihutubia katika maadhimisho hayo, aliwataka walimu kote nchini kuendelea kujituma na kujiendeleza kitaaluma ili kuhakikisha kuwa Tanzania inaendelea kutoa elimu bora yenye kuendana na mahitaji ya dunia ya sasa.

“Kazi ya ualimu ni kazi ya upendo na kujitoa kwa ajili ya ustawi wa wanafunzi wetu. Walimu ndiyo nguzo ya jamii na wanastahili pongezi kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kulea vizazi vya leo na vya kesho,” alisema Dkt. Kazungu.

Dkt. Kazungu aliwakumbusha walimu kuwa wanayo nafasi kubwa katika kuunda tabia, maadili na utu



Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dkt. Khatibu Kazungu, akihutubia walimu na wadau wa elimu katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani kilichofanyika katika Viwanja vya Kilimani jijini Dodoma tarehe 5 Oktoba, 2025.

wa wanafunzi, na kwamba mchango wao hauwezi kupuuzwa katika maendeleo ya taifa.

Alisisitiza kuwa walimu wazuri si wale wanaofundisha vitabu pekee, bali wale wanaootesha mbegu za maarifa na kuwasaidia wanafunzi kufikia uwezo wao kamili.

Kaulimbiu ya maadhimisho ya mwaka huu ilikuwa “Wezesha Walimu Kuchagua Viongozi Bora kwa Elimu na Mafunzo Stahiki”, kaulimbiu ambayo Dkt. Kazungu alisema inaendana vyema na mazingira ya sasa nchini, hasa kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025.

“Mwaka huu ni muhimu kwa mustakabali wa nchi yetu. Ni jukumu letu sote kuhakikisha tunawachagua viongozi watakaosimamia vyema sekta ya elimu na kuhakikisha walimu wanapata maslahi na mazingira bora ya kufanyia kazi,” aliongeza.

Aidha, Dkt. Kazungu aliipongeza serikali kwa kuendelea kuboresha sekta ya elimu kwa kujenga shule mpya, kuongeza ajira kwa walimu, na kuboresha miundombinu ya kufundishia.

Hata hivyo, alitoa wito kwa jamii na wazazi kushirikiana na serikali kuhakikisha kuwa walimu wanathaminiwa na kupewa rasilimali stahiki ili kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

“Serikali, wazazi na jamii kwa ujumla tunapaswa kushirikiana kuhakikisha walimu wanapata mazingira bora ya kufundishia na rasilimali zinazohitajika. Elimu bora haiwezi kupatikana bila mwalimu mwenye morali, taaluma na motisha,” alisema.

Dkt. Kazungu alihitimisha hotuba yake kwa kuwataka walimu kuendelea kuwa chachu ya mabadiliko katika jamii, akisisitiza kwamba Siku ya Mwalimu Duniani siyo siku ya mapumziko, bali ni siku ya kutafakari na kujipanga kufanya vizuri zaidi katika kazi yao tukufu ya kuelimisha taifa.



Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Bi Mariam Mnikwa akitoa salamu wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani kilichofanyika tarehe 5 Oktoba, 2025 katika viwanja vya Kilimani jijini Dodoma.

DKT. KAZUNGU AWAPONGEZA WALIMU KWA KUJITOA KUKUZA ELIMU – ATOA WITO WA KUCHAGUA VIONGOZI BORA WANAOSIMAMIA SEKTA YA ELIMU



Rais wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Dkt. Suleiman Ikomba akitoa salamu za chama hicho wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani kilichofanyika tarehe 5 Oktoba, 2025 katika viwanja vya Kilimani jijini Dodoma.



Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dkt. Khatibu Kazungu, akitoa tuzo kwa walimu walioshinda michezo mbalimbali katika bonanza la kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani katika Viwanja vya Kilimani jijini Dodoma tarehe 5 Oktoba, 2025.



Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dkt. Khatibu Kazungu, akisalimiana na wachezaji wa mpira wa pete katika bonanza la kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani katika Viwanja vya Kilimani jijini Dodoma tarehe 5 Oktoba, 2025.



Baadhi ya walimu kutoka shule mbalimbali za Mkoa wa Dodoma wakifuatilia hotuba ya mgeni rasmi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani.

BENKI YA NMB YAMTUNUKU CHETI CHA SHUKRANI KATIBU WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU



na kuendelea kuwa mstari wa mbele katika kuimarisha sekta ya kifedha nchini.

Alisema NMB imekuwa mshirika muhimu katika kutoa huduma zinazowagusa walimu moja kwa moja, ikiwemo mikopo, ushauri wa kifedha na uwekezaji.

"Tunafurahia kuona NMB ikiendelea kuwa benki ya mfano katika kuhudumia wateja wake kwa weledi na ubunifu. Tunahimiza wadau wengine wa kifedha kuiga mfano huu," alisema Nkwama.

Kaulimbiu ya Wiki ya Huduma kwa Wateja kwa mwaka huu ni "Huduma Bora, Wateja Wenye Furaha", ikilenga kuhimiza taasisi mbalimbali kuwathamini wateja na kuboresha huduma kila siku.

Wiki ya Huduma kwa Wateja ni maadhimisho ya kimataifa yanayofanyika kila mwezi Oktoba, ambapo taasisi mbalimbali husherehekea kwa kuonyesha upendo na shukrani kwa wateja wao.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati) akipokea cheti cha shukrani kutoka kwa Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Kambarage, Emiliana Mlay (kulia), wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Huduma kwa Wateja mkoani Dodoma. Kushoto ni Afisa Rasilimali Watu Mwandamizi Kanda ya Kati, Katengesya John.

Na Mwandishi Wetu, Dodoma.

Benki ya NMB Mkoa wa Dodoma imezindua rasmi Wiki ya Huduma kwa Wateja (Customer Service Week) kwa kufanya hafla fupi iliyofanyika katika Tawi la Kambarage, jijini Dodoma, ikiwa ni sehemu ya mkakati wake wa kuendelea kuboresha huduma na kuimarisha mahusiano na wateja wake.

Katika hafla hiyo, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama, alitunukiwa Cheti cha Shukrani na Benki ya NMB kama ishara ya kutambua mchango wake na ushirikiano mkubwa alioouonesha katika kuendeleza huduma bora za kifedha kwa walimu na watumishi wa umma.

Akizungumza katika hafla hiyo, Meneja wa Tawi la Kambarage, Bi. Emiliana Mlay, alisema Benki ya NMB itaendelea kutoa huduma bora, zenye ubunifu na zinazokidhi mahitaji ya wateja, huku ikisisitiza kuwa benki hiyo imedhamiria kubaki kuwa kinara katika utoaji wa huduma bora za kifedha nchini.

"Tunathamini wateja wetu wote, hasa wale wanaotupa ushirikiano wa karibu katika kukuza huduma zetu. Wiki hii ni ya kuonesha upendo, shukrani na kujifunza zaidi kutoka kwa wateja wetu," alisema Bi. Mlay.

Kwa upande wake, Mwl. Paulina Nkwama aliishukuru Benki ya NMB kwa kutambua mchango wa wateja wake



Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Kambarage, Emiliana Mlay (kushoto) akimlisha keki Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kulia) wakati wa hafla ya uzinduzi wa Wiki ya Huduma kwa Wateja jijini Dodoma.

BENKI YA NMB YAMTUNUKU CHETI CHA SHUKRANI KATIBU WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU



Mwl. Paulina Nkwama (katikati) akitoa neno la shukrani wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Huduma kwa Wateja ya Benki ya NMB jijini Dodoma. Kushoto ni Meneja wa Tawi la Kambarage, Emiliana Mlay, na kulia ni Katengesya John, Afisa Rasilimali Watu Mwandamizi wa benki hiyo.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na wafanyakazi wa Benki ya NMB na wateja wengine wakati wa uzinduzi rasmi wa maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja jijini Dodoma.

“MWALIMU NI CHIMBUKO LA KADA ZOTE NDANI NA NJE YA UTUMISHI WA UMMA,” – PROF. MURUKE AWATAKA WALIMU KUENDELEA KUIMARISHA ELIMU



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke akitoa neno la kumkaribisha mgeni rasmi kwenye kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Walimu Duniani tarehe 5 Oktoba, 2025 katika viwanja vya Kilimani jijini Dodoma.

Na Mwandishi Wetu – Dodoma.

Akizungumza kwenye kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Walimu Duniani tarehe 5 Oktoba 2025, Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke, aliwahimiza walimu nchini kujiheshimu, kuheshimiwa na kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu.

Prof. Muruke alitoa kauli hiyo katika Viwanja vya Kilimani jijini Dodoma wakati wa bonanza lililoandaliwa na Tume ya Utumishi wa Walimu na kuhuduriwa na walimu na wadau mbalimbali wa elimu ikiwa ni kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani.

“Napenda kuwapongeza walimu wote kwa mchango wenu mkubwa katika malezi, elimu na maendeleo ya taifa. Mwalimu ni chimbuko la kada zote ndani na nje ya Utumishi

wa Umma,” alisema Prof. Muruke, akisisitiza kwamba siku hiyo ni fursa ya kutambua hadhi ya walimu na mchango wao katika jamii.

Aidha, walimu walifurahia bonanza la michezo na mazoezi ya kukimbia (jogging) kutoka Bunge hadi Viwanja vya Kilimani, ikiwapa nafasi ya kubadilishana mawazo, kujenga mshikamano na kuimarisha afya zao.

Prof. Muruke aliwataka walimu kushiriki kikamilifu katika kujenga taifa, ikiwemo ushiriki katika uchaguzi mkuu, akisema walimu ni kioo cha jamii na wana nafasi ya kuhamasisha jamii kushiriki kwa amani na utulivu.

Alisisitiza kuwa maadhimisho hayo ni mwito wa kuenzi walimu, kuwawezesha na kuwatambua kama washiriki muhimu katika kuimarisha misingi ya demokrasia na maendeleo endelevu ya taifa.

“Tuwape walimu sauti na nafasi katika safari ya kujenga taifa imara lenye mshikamano wa kweli,” alimalizia Prof. Muruke.



Mwenyekiti wa Tume, Prof. Masoud Hadi Muruke (wa pili kutoka kulia), Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama (kushoto), Kamishna wa Tume, Bi. Maria Mnilwa (wa tatu kutoka kushoto) wakiongoza mazoezi ya kukimbia (jogging) kutoka Bunge hadi Viwanja vya Kilimani ikiwa ni kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Walimu Duniani tarehe 5 Oktoba, 2025 katika jijini Dodoma.

“MWALIMU NI CHIMBUKO LA KADA ZOTE NDANI NA NJE YA UTUMISHI WA UMMA,” – PROF. MURUKE AWATAKA WALIMU KUENDELEA KUIMARISHA ELIMU



Walimu wakipokea tuzo mbalimbali zilizotolewa na Tume ya Utumishi wa Walimu wakati wa bonanza lililowaleta pamoja katika viwanja vya Kilimani jijini Dodoma siku ya kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani tarehe 5 Oktoba, 2025.

“MWALIMU NI CHIMBUKO LA KADA ZOTE NDANI NA NJE YA UTUMISHI WA UMMA,” – PROF. MURUKE AWATAKA WALIMU KUENDELEA KUIMARISHA ELIMU



Walimu wakipokea tuzo mbalimbali zilizotolewa na Tume ya Utumishi wa Walimu wakati wa bonanza lililowaleta pamoja katika viwanja vya Kilimani jijini Dodoma siku ya kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani tarehe 5 Oktoba, 2025.

“MWALIMU NI CHIMBUKO LA KADA ZOTE NDANI NA NJE YA UTUMISHI WA UMMA,” – PROF. MURUKE AWATAKA WALIMU KUENDELEA KUIMARISHA ELIMU



Walimu wakipokea tuzo mbalimbali zilizotolewa na Tume ya Utumishi wa Walimu wakati wa bonanza lililowaleta pamoja katika viwanja vya Kilimani jijini Dodoma siku ya kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani tarehe 5 Oktoba, 2025.

“MWALIMU NI CHIMBUKO LA KADA ZOTE NDANI NA NJE YA UTUMISHI WA UMMA,” – PROF. MURUKE AWATAKA WALIMU KUENDELEA KUIMARISHA ELIMU



Walimu wakipokea tuzo mbalimbali zilizotolewa na Tume ya Utumishi wa Walimu wakati wa bonanza lililowaleta pamoja katika viwanja vya Kilimani jijini Dodoma siku ya kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani tarehe 5 Oktoba, 2025.

“MWALIMU NI CHIMBUKO LA KADA ZOTE NDANI NA NJE YA UTUMISHI WA UMMA,” – PROF. MURUKE AWATAKA WALIMU KUENDELEA KUIMARISHA ELIMU



Walimu wakipokea tuzo mbalimbali zilizotolewa na Tume ya Utumishi wa Walimu wakati wa bonanza lililowaleta pamoja katika viwanja vya Kilimani jijini Dodoma siku ya kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani tarehe 5 Oktoba, 2025.

TSC YAJADILI UTEKELEZAJI WA MRADI WA UJENZI DODOMA

Na Mwandishi wetu, Dodoma.

Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) tarehe 18 Septemba 2025 ilikutana na mkandarasi wa ujenzi, SUMA JKT, anayetekeleza mradi wa jengo jipya la Utawala la TSC Makao Makuu.

Kikao hicho kilichofanyika katika ukumbi wa Tume jijini Dodoma na kuongozwa na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama kililenga kujadili maendeleo na changamoto katika

utekelezaji wa mradi huo muhimu.

"Madhumuni makuu ya kikao chetu ni kufanya tathmini ya hatua zilizofikiwa hadi sasa na kuweka mikakati ya kuhakikisha mradi unakamilika kama ilivyopangwa. Mradi huu ni muhimu kwani utaboresha huduma za kiutumishi kwa walimu nchini," alisema Mwl. Nkwama.

Kwa upande wa SUMA JKT walieleza kuwa wanaendelea kufanya jitihada mbalimbali ili kuhakikishisha ubora na viwango

vya kitaalamu vinazingatiwa ili jengo hilo liwe la kisasa na la kudumu kwa matumizi ya muda mrefu.

Aidha, kikao hicho kilitoa fursa kwa pande zote mbili kujadili changamoto zinazojitokeza wakati wa utekelezaji na namna ya kuzitatua kwa haraka ambapo SUMA JKT iliahidi kuendelea kushirikiana kwa karibu ili malengo ya mradi yaweze kufikiwa.

Kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa jengo la Utawala la TSC unaotekelezwa katika eneo la Njedengwa jijini Dodoma kutaimarisha mazingira ya kazi na kuongeza ufanisi katika kutoa huduma bora kwa walimu na wadau wengine wa elimu nchini.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama, akiongoza kikao cha Menejimenti ya Tume na ujumbe kutoka SUMA JKT (harapo pichani) kilichofanyika tarehe 18 Septemba 2025 katika ofisi za TSC jijini Dodoma.



Baadhi ya wajumbe wa Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu wakiwa kwenye kikao na ujumbe kutoka SUMA JKT (harapo pichani) tarehe 18 Septemba 2025 katika ofisi za Tume jijini Dodoma.

TSC YAJADILI UTEKELEZAJI WA MRADI WA UJENZI DODOMA



Washiriki wa kikao kutoka SUMA JKT wakifuatilia majadiliano na Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu tarehe 18 Septemba 2025 jijini Dodoma.



Sehemu ya kikao kati ya Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu na ujumbe wa SUMA JKT kilichofanyika tarehe 18 Septemba 2025 jijini Dodoma.

MWL. NKWAMA AWAPONGEZA WALIMU WOTE NCHINI WAKATI WA MAADHIMISHO YA SIKU YA WALIMU DUNIANI



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu akitoa salamu wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Walimu Duniani jijini Dodoma tarehe 5 Oktoba, 2025.

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Walimu Duniani tarehe 5 Oktoba 2025, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu alitumia fursa hiyo kuwatakiwa walimu wote nchini na duniani heri ya maadhimisho, akisisitiza mchango wao mkubwa katika malezi, mafunzo na ujenzi wa kizazi chenye maarifa, maadili na

uzalendo.

Akizungumza kwenye sherehe zilizofanyika Viwanja vya Kilimani, Katibu wa Tume alibainisha kaulimbiu ya mwaka huu ya kimataifa, "Recasting teaching as a collaborative profession", inasisitiza umuhimu wa taaluma ya ualimu kama kazi ya ushirikiano.

Aidha, akizingatia uchaguzi mkuu utakaofanyika tarehe 29 Oktoba

2025, alihimiza walimu kushiriki kikamilifu kuchagua viongozi bora watakoleta maendeleo ya kweli katika sekta ya elimu.

Mwl. Nkwama alisisitiza kuwa Tume ya Utumishi wa Walimu inaendelea kushirikiana na walimu kuhakikisha haki zao za kiutumishi zinadumishwa, mazingira ya kazi yanaboreshwa, na maadili ya taaluma yanazingatiwa.



Katibu Tarwala wa Mkoa wa Dodoma, Dkt. Khatibu Kazungu (Katikati) akiwa meza kuu na viongozi mbalimbali wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani tarehe 5 Oktoba, 2025 jijini Dodoma.

MWL. NKWAMA AWAPONGEZA WALIMU WOTE NCHINI WAKATI WA MAADHIMISHO YA SIKU YA WALIMU DUNIANI



Burudani ya nyimbo ikiwa inaendelea wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani tarehe 5 Oktoba, 2025 jijini Dodoma.



Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dkt. Khatibu Kazungu akizungumza na wachezaji wa mpira wa pete kabla ya mchezo kuanza wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani tarehe 5 Oktoba, 2025 jijini Dodoma.

Viongozi wakielekea kwenye ukaguzi wa timu za michezo wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani tarehe 5 Oktoba, 2025 jijini Dodoma.



Walimu wakiwa katika hali ya furaha wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani tarehe 5 Oktoba, 2025 jijini Dodoma.

Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Mwl. Fatuma Muya (kushoto) akiwa na washiriki wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani tarehe 5 Oktoba 2025 katika viwanja vya Kilimani jijini Dodoma.

MAONESHU YA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA MWALIMU DUNIANI KATIKA VIWANJA VYA NYERERE SQUARE JIJINI DODOMA



Picha mbalimbali za maonesho yaliyoandaliwa na Tume ya Utumishi wa Walimu na kuhusisha wadau mbalimbali wa elimu yakiwa yanaendelea katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma. Maadhimisho hayo yalifanyika tarehe 1-5 Oktoba, 2025.

MAONESHU YA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA MWALIMU DUNIANI KATIKA VIWANJA VYA NYERERE SQUARE JIJINI DODOMA



Picha mbalimbali za maonesho yaliyoandaliwa na Tume ya Utumishi wa Walimu na kuhusisha wadau mbalimbali wa elimu yakiwa yanaendelea katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma. Maadhimisho hayo yalifanyika tarehe 1-5 Oktoba, 2025.

TSC TEMEKE YATOA KONGOLE KWA RAIS SAMIA KWA UTATUZI WA CHANGAMOTO ZA WALIMU



Na Mwandishi Wetu – Temeke

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Temeke imeipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jitihada kubwa za kutatua changamoto mbalimbali zilizokuwa zikiwakabili walimu na watumishi wa umma kwa ujumla.

Kauli hiyo imetolewa na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Temeke, Bw. Mohamed Salim, wakati wa mahojiano maalum na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, alipokuwa akielezea mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuboresha maslahi na mazingira ya kazi kwa walimu.

Bw. Salim alisema kuwa moja ya mafanikio makubwa ya Serikali ni kupunguza upungufu wa walimu, ambapo katika kipindi cha hivi karibuni walimu 233 wameajiriwa wilayani humo, wakiwemo walimu 63 wa shule za msingi na walimu 170 wa shule za sekondari.

Aidha, alieleza kuwa Serikali imeendelea kusimamia kwa ufanisi upandishwaji wa vyeo kwa walimu wenye sifa, jambo lililosaidia kupunguza malalamiko yaliyokuwa yakitolewa miaka ya nyuma.

“Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, walimu 2,291 walipandishwa vyeo, mwaka 2021/2022 walikuwa 1,378, mwaka 2022/2023 walikuwa 948, na mwaka 2023/2024 walifikia 2,830, wakiwemo walimu 10 waliopandishwa cheo zaidi ya kimoja,” alifanua Bw. Salim.

Ameongeza kuwa katika mwaka wa fedha 2024/2025, jumla ya walimu 599 wamepandishwa vyeo, wakiwemo walimu 403 wa shule za msingi na walimu 196 wa shule za sekondari.

Akizungumzia masuala ya stahiki za watumishi, Bw. Salim alisema kuwa Serikali imeendelea kulipa madai ya

likizo kwa walimu kwa wakati, ambapo kwa kipindi cha Juni 2021, walimu 449 walilipwa shilingi milioni 124.6, na mwezi Juni 2022 walimu 386 walilipwa shilingi milioni 123.5.

“Mwaka wa fedha 2020/2021 walimu 449 walilipwa shilingi milioni 99.8, na mwaka 2021/2022 walimu 761 walilipwa shilingi milioni 235.4. Haya yote ni mafanikio makubwa yanayoonesha dhamira ya Serikali ya kumtendelea haki mwalimu,” alisisitiza.

Vilevile, Bw. Salim alisema kuwa Serikali imetoa mafunzo kwa watumishi wa TSC nchini ili kuboresha utendaji kazi na kuwahudumia walimu kwa ufanisi zaidi. Pia, walimu wapya 233 walioajiriwa mwaka 2024/2025 walipewa mafunzo elekezi kabla ya kuanza majukumu yao.

TSC Wilaya ya Temeke pia imemshukuru Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama, kwa kuendelea kumsaidia Rais Samia katika kusimamia utekelezaji wa sera na maamuzi yanayolenga kuboresha ustawi wa walimu nchini.

Bw. Salim aliongeza kuwa kwa mwaka 2024/2025, Halmashauri ya Wilaya ya Temeke ilisajili walimu 262 wapya — walimu 72 wa shule za msingi na walimu 188 wa sekondari, hatua inayolenga kuziba pengo la upungufu wa walimu wilayani humo.

Aidha, alibainisha kuwa TSC imekuwa ikiendelea kutoa elimu ya maadili na utumishi wa umma kwa walimu, wakuu wa shule na viongozi wa elimu, kupitia mafunzo na vipeperushi vinavyotoa mwongozo wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Walimu.

“Tunawahimiza wakuu wa shule kuchukua hatua stahiki kwa makosa yaliyo ndani ya mamlaka zao, kama inavyoelekezwa na Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu ya mwaka 2015, sura ya 448, na Kanuni za mwaka 2016,” alisema.

Kwa sasa, Wilaya ya Temeke ina jumla ya shule 126 — shule 88 za msingi na shule 38 za sekondari — zenye jumla ya walimu 5,052, kati yao walimu 3,237 wa shule za msingi na walimu 1,815 wa sekondari.

Bw. Salim alihitimisha kwa kusema kuwa juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita zimeleta matumaini mapya kwa walimu na zimeongeza ari ya kufanya kazi kwa bidii, uadilifu na kujituma kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

TSC TEMEKE YATOA KONGOLE KWA RAIS SAMIA KWA UTATUZI WA CHANGAMOTO ZA WALIMU




TSC TEMEKE YATOA KONGOLE KWA RAIS SAMIA KWA UTATUZI WA CHANGAMOTO ZA WALIMU



Maafisa Urumishi kutoka TSC Temeke Bw Mohamed pamoja na Madam Tasana wakiwa katika Semina ya Walimu ajira mpya 2025.



Watumishi wa ofisi ya TSC Temeke katika picha ya pamoja.



Afisa Maadili Madam Bernadetha akiwa katika majukumu yake TSC Temeke



Afisa Rasilimali watu mkuu Daraja la kwanza Bw Mohammed akitoa elimu kwa Maafisa Utumishi katika ofisi za TSC Temeke.

TUME YA UTUMISHI WA WALIMU YAPONGEZWA KWA MAFUNZO YA WAJUMBE WA KAMATI ZA AJIRA, UPANDISHAJI VYEO NA NIDHAMU



Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dkt. Khatibu Kazungu (Katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi na washiriki wa bonanza la michezo katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani lililofanyika tarehe 5 Oktoba katika vifwanja vya Kilimani jijini Dodoma.

TUME YA UTUMISHI WA WALIMU YAPONGEZWA KWA MAFUNZO YA WAJUMBE WA KAMATI ZA AJIRA, UPANDISHAJI VYEO NA NIDHAMU



Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dkt. Khatibu Kazungu (Katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi na washiriki wa bonanza la michezo katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani lililofanyika tarehe 5 Oktoba katika viwanja vya Kilimani jijini Dodoma.

TUME YA UTUMISHI WA WALIMU YAPONGEZWA KWA MAFUNZO YA WAJUMBE WA KAMATI ZA AJIRA, UPANDISHAJI VYEO NA NIDHAMU



Wachezaji wa mpira wa miguu wakishangilia baada ya kushinda katika mchezo uliofanyika katika viwanja vya Kilimani jijini Dodoma ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani tarehe 5 Oktoba, 2025.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu